

Mai 1, 2020

Wapendwa Familia za JCPS,

Tumefikia zaidi ya nusu ya kumaliza kipindi cha Masomo Yasiyo ya Kiasili (NTI). Kuna siku 18 za shule zilizobaki katika mwaka wetu wa shule ambao umepangwa kumalizaka mnano Mai 27. Tunapenezwa sana jinsi wewe na kila mtu mwingine katika familia ya JCPS amebeba hii “mbinu mpya” ya kuelimisha watotot wetu nyumbani. Ushirika katika NTI umekuwa vyema zaidi ya 90%, kumaanisha karibu kila mwanafunzi anahusiana na mwalimu/walimu wao kila wiki. Hapa kuna habari kadhaa mpya:

- Mili: Wafanyikazi wetu wa Huduma ya Lishe wamesambaza zaidi ya milo 700,000 kwa wanafunzi tangu shule zifungwe mnamo Machi 13. Baadhi ya viwanda vya usambazaji vimebadilika au vitabadilika Jumatatu: Shule ya Msingi ya Jacob na Shule ya Upili ya Shawnee zimefungwa. Kiwanda cha Shawnee kimehamia Shule ya Msingi ya Young, Shuke ya Msingi ya Maupin imehamia Shule ya Msingi ya J.F. Kennedy na Shule ya Msingi ya Hazelwood imehamia Shule ya Upili ya Iroquois haya yote kwa sababu ya majengo na ufundi wa shule. Hii ni [orodha ya baadhi ya viwanda vya chakula](#).
- Vifurushi vya Karatasi: Wakati mwingine wa vifurushi vilivyo na chapa za karatasi za wiki mbili za bidhaa za maagizo zinapatikana sasa katika viwanda hivi 15 vya chakula: Kituo cha Jamii cha Americana, Blue Lick, Brandeis, Chancey, Crums Lane, Engelhard, Fern Creek, Frayser, Indian Trail, McFerran, St. Matthews, Shule za Upili za Wheatley na Young; Shule ya Kati ya Carrithers; na Shule ya Upili ya Valley. Unaweza pata bidhaa hizo hizo katika [ukurasa huu wa wavuti](#) au kuomba kufurushi kutumwe kwako kwa kupiga simu shule ya mtoto wako na kuwacha ujumbe.
- Mitihani ya AP: Kuna baadhi ya nafasi kubwa kwa wanafunzi wanaofanya mitihani ya AP mwaka huu. Wanafunzi wanaweza kufanya mitihani kutoka nyumbani Mai 11 hadi 22. Ratiba na maelezo yanaweza kupatikana kwenye [tovuti ya College Board](#).
- Simu ya UTUNZAJI: Kuanzia Jumatatu, familiza wanaweza kupiga simu 313-CARE (2273) kwa msaada na rufaa unaohusika na huduma za matibabu, msaada wa madawa ya kulevya na pombe, ukosefu wa makazi na mahitaji ya msingi kama chakula, makazi na matumizi. Simu hiyo ya UTUNZAJI itashughulikiwa na wataalam kutoka Idara ya Mipango ya Msaada wa Taaluma na inajumuisha washauri wa shule, watendaji wa afya ya akili, waratibu wa Huduma za Raslimali ya Familia na Vijana, na waratibu kutoka idara za Utoto, Huduma za Afya na Misaada ya Jamii.
- Darasa la Utambuzi la 2020: JCPS inaendeleza mipango kadhaa ya kusherehekea wakubwa wetu. Tayari tunashughulikia video za kila mmoja ya darasa zetu 28 za wakubwa. Tutakuwa na habari zaidi katika siku zijazo.

Usisahau kutufuata katika on [Facebook](#), [Twitter](#) na Instagram (@JCPSKY) kwa habari mpya za JCPS na sasisho. Tafadhali shiriki picha zako za NTI na sisi na utumie alama ya reli #WeAreJCPSAtHome na #ThisIsHowINTI ili kutusaidia kuendelea kuhimiza wanafunzi wetu wakati tunaendelea kubaki Wenye Afya Nyumbani.